TAARIFA YA IDARA YA AFYA KWA KIPINDI CHA KUANZIA OKTOBA HADI DESEMBA 2016/2017.

Mkuu wa Idara ya Afya aliwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Idara ya Afya katika kipindi cha robo ya pili kwa Mwaka wa fedha 2016.

i. <u>IDADI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA:</u>

Jedwali Na:1

AINA	IDADI	MMILIKI			
		SERIKALI	TAASISI ZA UMMA	MASHIRIKA YA DINI	BINAFSI
Hospitali	1	1	0	0	0
Kituo cha Afya	1	1	0	0	0
Zahanati	33	31	1	0	1
Jumla	**35**	**33**	**1**	**0**	**1**

2. <u>MADAWA NA VIFAA TIBA</u>.

Katika kipindi cha Robo ya Pili kwa mwaka wa fedha,2016/ 2017 Idara ya Afya ilinunua Dawa na Vifaa tiba MSD,kupitia Mfuko wa pamoja wa Wahisani (Basket Funds) kiasi cha Tsh 60,024,660/= pia idara ilipata mgao wa dawa na vifaa tiba kutoka MSD kiasi cha Tsh 10,678,100/=

i: <u>HOSPITALI</u>

Jedwali Na:2

AINA	THAMANI
Dawa mchanganyiko na vifaa tiba	**43,735,160/=**

ii: <u>KITUO CHA AFYA</u>

Jedwali Na:3

AINA	THAMANI	USAMBAZAJI
Dawa mchanganyiko na viffaa tiba	**5,646,200.00**	ulifanywa na Bohari ya madawa MSD/Mganga mkuu

iii: ZAHANATI

Jedwali Na:4

AINA	THAMANI	USAMBAZAJI
Dawa mchanganyiko na vifaa tiba.	**21,321,400.00**	Ulifanywa na Bohari ya madawa MSD/Mganga mkuu

3. <u>HUDUMA ZA MAABARA</u>.

Huduma zilizotolewa katika kitengo cha Maabara ni kama zifuatazo:

Jedwali Na: 4

NA	AINA YA KIPIMO	IDADI YA WAGONJWA	MATOKEO
1	Choo (haja kubwa)	136	Wagonjwa 4 waliyogundulika kuwa na minyoo
2	Mkojo	2030	Wagonjwa 58 walikutwa na maambukizi ya ugonjwa wa kichocho.

3	Makohozi kwa ajili ya TB	81	Wagonjwa 7 waligundulika kuwa na vimelea hivyo vya kifua kikuu(TB)
4	Kaswende(RPR)	48	Wagonjwa 2 walikutwa wana vimilea vya ugonjwa huo
5	Wekundu wa damu (HB)	3420	Wagonjwa 480 waligundulika kuwa na HB chini 50%
6	Makundi ya damu (A,B,O Blood grouping)	473	Jumla ya watu 173 waliweza kuchangia damu kwa ndugu zao.
7	Kinga mwili CD4	65	Wagonjwa 22 waligundulika kuwa na CD4 chini ya 350
8	Damu kwa ajili ya Kiasi cha Sukari	16	Hakuna Mgonjwa aliyegundulika kuwa na ugonjwa wa kisukari
9	Mkojo kwa ajili ya Kiasi cha Sukari	52	Hakuna mgonjwa aliyegundulika kuwa na kisukari
10	Mkojo kwa ajili ya ` Ujauzito	157	Akina mama 79 waligundulika kuwa na ujauzito.
11	Hepatits B	0	Wagonjwa 0 waligundulika na matatizo. o/s
12	Hepatits C	0	Hakuna mgonjwa aliyegundulika na tatizo.0 o/s
13	Upimaji wa hamirojo kwenye mkojo	162	Wagonjwa 41 waligundulika kuwa na hamirojo kwenye mkojo.
14	Kipimo cha kuangalia uchafu wa damu “ESR”	21	Wagonjwa 3 waligundulika na matatizo (ESR).
15	Kipimo cha kuangalia uwezo wa damu kuganda kabla ya upasuaji.	0	Hakuna aliyegundulika na tatizo.
16	Kizio kikubwa cha Damu	413	Waliogundulika na matatizo ni 57.
17	Kipimo cha malaria kwenye Damu	4108	1096 waligundulika kuwa na Malaria

4. <u>HUDUMA YA MACHO</u>.

(i)Idadi ya wagonjwa waliofika kupata huduma.

Jedwali Na:5

Na		**> ya Miaka5**			**< ya Miaka5**			**Jumla**		
		Me	**Ke**	**Jumla**	**Me**	**Ke**	**Jumla**	**Me**	**Ke**	**Jumla**
1	Wapya	5	8	13	33	36	69	38	44	82
2	Waliofuatiliwa	1	0	1	0	0	0	1	0	1
	Jumla	**6**	**8**	**14**	**33**	**36**	**69**	**39**	**44**	**83**

5. <u>MAGONJWA 10 YALIYOONGOZA KWA WAGONJWA WA NJE (OPD)</u>

<u>Jedwali Na: 6</u>

Na	**AINA YA UGONJWA**	**IDADI YA WAGONJWA**
1.	Malaria	4439
2.	Magonjwa ya njia ya hewa	3776
3.	Kuharisha	1224

4	Kichomi	497
5	Magonjwa ya macho	796
6	Homa ya mapafu	3776
7	Minyoo	361
8	Mkojo (UTI)	627
9	Upungufu wa Damu	92
10	Magonjwa ya Ngozi	435

6. MAGONJWA 10 YALIYOONGOZA KWA WAGONJWA WALIOLAZWA PAMOJA NA IDADI YA WAGONJWA WALIOFARIKI .

Jedwali Na: 7

Na	AINA YA UGONJWA	WALIOLAZWA	WALIOFARIKI
1	Malaria	88	8
2	Upungufu wa damu	45	0
3	Kuharisha	14	0
4	Magonjwa ya njia ya mkojo (UTI)	36	0
5	Kichomi	8	3
6	Ajali barabarani	4	0
7	Magonjwa ya moyo	3	2
8	Kifua Kikuu	2	2
9	Ukimwi (Magonjwa nyemelezi)	10	0
10	Magonjwa ya njia ya hewa	2	0

7.HUDUMA YA UPASUAJI.

Jedwali Na:8

Na	AINA YA UPASUAJI	IDADI
1.	Upasuaji mkubwa	134
2.	Upasuaji mdogo	97
3.	Ufungaji kizazi	18
4	Kusafisha Masikio	13
5	Kutahiri watoto wa kiume	4
6	Kunyoosha miguu, mikono, na kufunga POP	40

8. HUDUMA ZA X-RAY.

Jedwali Na:9

Na	AINA YA PICHA ZILIZOPIGWA	IDADI
1.	Kifua	73
2.	Miguu	35
3.	Mikono	54
4.	Fuvu la kichwa	3
5.	Tumbo	5
6.	Uti wa mgongo	9
7.	Nyonga	4
	Jumla ya wagonjwa wote	**183**

9. HUDUMA YA CHANJO.

Jedwali Na: 10

AINA YA CHANJO	LENGO	WALIOCHANJWA	KIWANGO %
Kifua Kikuu	888	568	63.96
Homa ya Kupooza (Polio) 0	888	547	62

Polio 1	888	560	63
Polio 2	888	540	60
Polio 3	888	527	65
Pental 1	888	576	64
Pental 2	888	561	63
Pental 3	888	535	60
Surua 1	888	552	62
Surua 2	888	267	30
Pepo punda 1	888	373	42
Pepo Punda 2	888	279	31
PCV 13- 1	888	572	64
PCV 13- 2	888	551	62
PCV 13- 3	888	524	59
Rota 1	888	563	63
Rota 2	888	560	63

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi hiki Idara imenunua Mitungi 105 na kuisambaza katika vituo vya kutolea huduma na kuisambaza katika vituo vya kutolea huduma ya Afya, pia tumetengeneza Jokofu la Mirui.

10. <u>UZAZI</u>.

Jedwali Na: 11

JUMLA YA HUDUMA ZA UZAZI ZILIZOTOLEWA.	**AINA YA UZAZI**								
	Kujifungua kawaida	Kujifungua kwa kupasuliwa	Kutanguliza matako	Waliozaliwa wafu wamechubuka	Waliozaliwa wafu hawakuchubuka	Waliozaa mapacha	Waliozaliwa na uzito chini ya kg 2.5	Mimba zilizoharibika	Waakina mama waliofariki wakati wa kujifungua
	495	**94**	**8**	**11**	**7**	**15**	**55**	**43**	**00**

<u>TAARIFA YA ROBO YA MWAKA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KITENGO CHA USTAWI WA JAMII KATIKA IDARA YA AFYA KUANZIA OKTOBA-DISEMBA 2016 KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE</u>.

i. HUDUMA YA MSAMAHA WA MATIBABU KWA MAKUNDI MAALUMU AMBAYO NI WAZEE WASIOJIWEZA NA WA MAGONJWA SUGU.

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi husika ofisi ya ustawi wa Jamii –idara ya Afya imefanikiwa kuratibu misamaha ya matibabu kwa watu wapatao 29 kutoka katika makundi maalumu ambayo ni wazee wasiojiweza, walemavu na wale wenye magonjwa sugu. Ifuatayo ni orodha ya watu husika waliopata msamaha wa matibabu kwa kipindi tajwa hapo juu.

S/N	**JINA KAMILI**	**UMRI**	**JINSI**	**KIJIJI ATOKACHO**
1	Abdala Mohamedi Mputo	78	ME	Mangirikiti

2	Zainabu Mshamu Ngwate	18	KE	Likongowele
3	Maisha Kassim Mbugila	10	KE	Mbonde
4	Chande Mulyango	80	ME	Mbuli
5	Zubeda Tewele	32	KE	Ngongowele
6	Silvia Stanley Matola	24	KE	Hulia
7	Mshamu Aly Lipala	76	ME	Mihumo
8	Zuhura Abdala Ngachengela	63	KE	Makonjiganga
9	Halima Mohamedi Ngalinga	85	KE	Nangando
10	Sudi Chande Mnemba	36	ME	Kiangara
11	Sadamu Saidi Kipepe	9	ME	Mkundi
12	Darlini Mbinga	31	KE	Ngorngopa
13	Amina Rashidi Mmambe	65	KE	Likongowele
14	Fatuma Mohamedi Kawembe	82	KE	Likongowele
15	Rajabu Ibraimu Ndeo	70	ME	Mirui
16	Gaudensia John	65	KE	Liwale B
17	Daima Kipangila	73	ME	Nabuya
18	Mwanahawa Abdala Huki	75	KE	Likongowele
19	Kasimu Indiwa	80	ME	Likombora
20	Mwanahawa Libihi	79	KE	Barikiwa
21	Jafari Ally Tewele	83	ME	Nangando
22	Zainabu .B. Manuu	55	KE	Likongowele
23	Hemed Mohamedi Ngajaja	80	ME	Kikyulungu
24	Kassimu Ally Kumbota	85	ME	Kitogoro
25	Esha Mpinge	71	KE	Muungurumo
26	Abibu Abdala Makanga	57	ME	Mikunya
27	Saidi Kilima	90	ME	Naluleo
28	Baitina Mohamedi Mausesi	84	KE	Muungurumo
29	Luca Matosa Litawa	85	ME	Muungurumo

ii. HUDUMA YA USTAWI WA FAMILIA NA WATOTO; MALEZI NA MAKUZI KWA WATOTO PAMOJA NA HUDUMA ZA USULUISHI WA NDOA.

Taarifa za huduma hizo ni Usuluhishi wa ndoa zenye mfarakano(matrimonial) na matunzo kwa watoto walio kwenye ndoa zenye mfarakano.

Halmashauri	Aina ya mashauri.	Idadi ya mashauri yaliopelekwa ofisi ya u/wa jamii.	Idadi ya mashauri yaliyo suluhishwa.	Idadi ya mashauri yaliopelekwa mahakamani.	Sababu za migogoro ya ndoa	
					Utunzaji wa watoto	Mali
Liwale	Unyumba	0	0	0		
	matunzo	35	26	9	32	3
JUMLA		**35**	**26**	**9**	**32**	**3**

iii. ELIMU NA UHAMASISHAJI KWA JAMII JUU YA UCHANGIAJI WA HIALI WA DAMU:

Taarifa ilieleza kuwa kipindi husika Ofisi ya ustawi wa jamii kwa kushiikiana na Timu ya **DAMU SALAMA** wilaya imeweza kutoa elimu na uhamasishaji kwa jamii juu ya suala la kujitolea katika kuchangia damu inayohitajika katika hospitali ya wilaya kwa wagonjwa mbalimbali hususani akina mama wajawazito,watoto na wagonjwa wengineo. Na katika kipindi hiki uhamasishaji wa kuchangia damu kwa hiali ulifanyika katika shule ya *sekondari Anna magowa* na chupa za damu zipatazo 17 zilikusanywa.

iv. UKATILI WA KIJINSIA NA UKATILI DHIDI YA WATOTO;

Halma shauri	**Aina ya ukatili**		**Watu wazima**		**Jumla**	**Watoto**		**Jumla**
			Me	**Ke**		**Me**	**Ke**	
Liwale	Ukatili wa kudhuru mwili	Kukatwa kiungo	0	0	**0**	1	0	**1**
		Kuchomwa moto	0	0	**0**	0	0	**0**
		ukeketaji	0	0	**0**	0	0	**0**
		Kipigo kikali mwilini	0	0	**0**	0	0	**0**
		Kuchomwa kitu chenye ncha kali	0	0	**0**	0	0	**0**
	Ukatili wa kingono	kubakwa	0	0	**0**	0	0	**0**
		kulawitiwa	0	0	**0**	3	0	**3**
		Kunajisi wachanga	0	0	**0**	0	0	**0**

		Madhara sehemu za siri (kwa kitu chenye ncha kali)	0	0	**0**	0	0	**0**
	Ukatili wa kisaikolojia		0	0	**0**	0	0	**0**
	Ukatili wa kiuchumi		0	0	**0**	0	0	**0**
	Ukatili wa kutelekezwa		0	0	**0**	16	19	**35**

v. MAKUNDI MAALUMU (WAZEE, WALEMAVU NA WATOTO WAISHIO KATIKA MAZINGIRA HATARISHI (MVC).

Katika kipindi tajwa hapo juu ofisi ya Ustawi wa Jamii-idara ya Afya imeweza kuyatambua makundi maalum na kuhuisha takwimu za wazee,walemavu na watoto waishio katika mazingira hatarishi (MVC) kwa kushirikiana na watendaji wa vijiji na kata ili kupata takwimu kamili za makundi hayo,hivyo basi makundi hayo maalumu yameshatambuliwa .Vifuatavyo ni vielelezo vinavyoonyesha mchanganuo wa takwimu za makundi maalumu.

- **Idadi ya watoto walio katika mazingira hatarishi(MVC) waliotambuliwa.**

WILAYA	**IDADI YA KATA**	**IDADI YA VIJIJI**	**IDADI YA MVC**		
			KE	**ME**	**JUMLA KUU**
LIWALE	20	76	1541	1765	5307

- **Huduma zilizotolewa kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi(MVC)**

WILAYA	**IDADI YA KATA**	**AINA YA HUDUMA**	**IDADI YA WATOTO WAISHIO MAZINGIRA HATARISHI NA HUDUMA WALIZOPEWA**
LIWALE	10 (Liwale Mjini,Likongowele,Nangando,Liwale B,Mihumo,Barikiwa,Mbaya,Kiangara,Kibutuka na Makata)	AFYA (CHF)	2340
		CHAKULA	105
		MADAFTALI,PENI	68
		VYETI VYA KUZALIWA	41

WATU WENYE ULEMAVU:

- **Idadi ya watu wenye ulemavu waliotambuliwa**

WILAYA	**IDADI YA KATA**	**IDADI YA VIJIJI**	**IDADI YA WALEMAVU**		
			KE	**ME**	**JUMLA KUU**
LIWALE	20	76	689	873	1562

WAZEE:

- **Idadi ya wazee (ME na KE) waliotambuliwa katika wilaya yetu**

WILAYA	IDADI YA KATA	IDADI YA VIJIJI	IDADI YA WAZEE		
			KE	ME	JUMLA KUU
LIWALE	20	76	2807	2500	5307

- **Idadi ya mabalaza ya wazee yalioanzishwa.**

WILAYA	IDADI YA WILAYA	IDADI YA KATA	IDADI YA VIJIJI	IDADI YA MABARAZA YA WAZEE. JUMLA KUU.
LIWALE	1	20	76	98

vi. HUDUMA KWA WALEMAVU

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi tajwa hapo juu ofisi iliweza kuwawezesha baadhi ya walemavu na wazee kuhudhuria katika makongamano ya kitaifa yaliyofanyika mkoani Mbeya na kuratibu kikao cha watu wenye ulemavu ambacho kilifanyika katika ofisi ya ustawi wa jamii kwa lengo la kuwakutanisha pamoja walemavu hao ili waweze kupanga na kujadiliana juu ya masuala yao yanayowahusu kwa ajili ya ustawi wao.

CHANGAMOTO

Pamoja na utekelezaji wa shughuli za Ustawi wa Jamii kitengo hiki kimekuwa kikika.
biliwa na changamoto zifuatazo.
-Usafiri kuifikia jamii tatizo.
-Fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za ofisi kutokana na ufinyu wa bajeti ya Ustawi wa Jamii.
-Kutokuwepo kwa Maafisa Ustawi wa Jamii wa kutosha sawia na majukumu yaliyopo.

12.TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO YA PILI MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA.

Katika kipindi cha robo ya pili kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 taarifa ya fedha Salio anzia ni **Tsh.58,159,321.55**,Fedha zilizokusanywa (Bima ya afya,CHF na Papo kwa papo) ni **Tsh 22,133,140.00,** jumla ya fedha zote (Salio anzia,Bima ya afya,CHF na Papo kwa papo) ni **Tsh 80,292,461.55**,Fedha zilizotumika ni**Tsh. 18,184,472.00,** na fedha zilizosalia (Bakaa) ni **Tsh.50,286,964.55** Mchanganuo huu umeainishwa katika kiambatanisho **"A".**

KIAMBATANISHO "A"

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI HOSPITAL YA (W)

NA KITUO CHA AFYA ,ZAHANATI MWEZI OKTOBA-DISEMBA 2016.								
KITUO	**SALIO**	**BIMA YA AFYA**	**CHF**	**PAPO KWA PAPO**	**MENGINEYO**	**JUMLA**	**MATUMIZI**	**BAKAA**
LIWALE HOSPITALI (W)								
COST SHARING:	494,242.14	5,019,680.00	2,450,000.00	4,991,000.00	1,634,900.00	17,039,822.00	13,308,450.00	3,731,372.14
DRUG REV. FUND:	1,474,440.27	-	-	3,705,470.00	-	5,179,910.27	2,804,930.00	2,374,980.27
KIBUTUKA	445,336.44	-	-	300,000.00	-	745,336.44	195,000.00	550,336.44
LILOMBE	15,555,357.61	253,040.00	365,000.00	-	-	2,173,392.61	370,000.00	1,803,052.61
MAKATA	3,378,929.99	32,245.00	230,000.00	-	-	3,641,174.99	-	3,641,174.99
NGONGOWELE	1,471,962.23	77,280.00	-	-	-	1,549,242.23	-	1,549,242.23
MLEBWE	2,847,563.22	-	80,000.00	59,000.00	-	2,986,563.22	-	2,986563.22
NDUNYUNGU	189,465.43	-	-	-	-	189,465.43	-	189,465.43
NANGANO	297,162.91	-	80,000.00	-	-	377,162.91	8,732.00	368,430.91
NAUJOMBO	2,203,883.68	-	-	16,500.00	-	2,220,383.68	-	2,220,383.68
KIKULYUNGU	898,430.00	61,885.00	40,000.00	-	-	1,000,315.00	223,000.00	777,315.00
KIMAMBI	1,269,024.00	-	-	-	-	1,269,024.00	-	1,269,024.00
NGUNJA	3,457,436.25	163,270.00	100,000.00	-	-	3,720,706.25	-	3,720,706.25
MANGIRIKITI	727,764.00	-	435,000.00	-	-	1,162,764.00	-	1,162,764.00
KIPELELE	652,332.00	-	-	-	-	652,332.00	11,800.00	640,532.00
NDAPATA	110,552.75	-	-	-	-	110,552.75	-	110,552.75
MIKUNYA	1,653,655.89	37,590.00	-	-	-	1,691,245.89	243,540.00	1,447,705.89
NAHORO	2,222,747.00	-	30,000.00	-	-	2,252,747.00	-	2,252,747.00
KIPURE	965,105.45	23,445.00	40,000.00	58,600.00	-	1,087,150.45	-	1,087,150.45
LIWALE B	3,273,374.00	58,050.00	-	-	-	3,273,374.00	-	3,273,374.00
MPIGAMITI	1,202,526.50	-	-	9,000.00	-	1,211,526.50	-	1,211,526.50
KITOGORO	939,437.61	-	-	-	-	939,437.61	290,000.00	649,437.61

MPENGELE	1,263,980.61	-	145,000.00	26,500.00	-	1,435,480.61	-	1,435,480.61
MKUTANO	290,942.89	-	-	-	-	290,942.89	-	290,942.89
MIRUI	2,813,928.04	127,045.00	2,490,000.00	-	-	5,430,973.04	-	5,430,973.04
KIANGARA	1,687,363.53	27,210.00	110,000.00	12,000.00	-	1,836,573.53	-	1,836,573.53
BARIKIWA	1,571,039.00	39,040.00	130,000.00	-	-	1,740,079.00	-	1,740,079.00
NGUMBU	574,461.00	-	-	-	-	574,461.00	-	574,461.00
MIHUMO	2,272,331.30	-	150,000.00	-	-	574,461.30	-	574,461.30
MBAYA	556,503.33	32,900.00	-	-	-	589,403.33	250,000.00	339,403.33
NAMIHU	363,044.45	-	-	-	-	363,044.45	-	363,044.45
LIKOMBORA	155,705.57	27,080.00	-	-	-	182,785.57	-	182,785.57
KICHONDA	723,586.89	-	-	-	-	723,586.89	466,880.00	256,706.89
MTAWANGO	155,705.57	20,310.00	80,000.00	-	-	256,015.57	11,800.00	244,215.57
TOTAL	**58,159,321.55**	**6,000,000.00**	**6,955,000.00**	**9,178,070.00**	**1,634,900.00**	**68,471,436.55**	**18,184,472.00**	**50,286,964.55**

5. IDARA YA MAJI

Mkuu wa Idara ya Maji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za Idara ya Maji kwa kipindi Oktoba hadi Disemba , 2017. Taarifa ilieleza kuwa Idara ya maji katika kipindi cha robo ya pili, Oktoba hadi Disemba , imefanya shughuli mbali mbali pamoja na ukarabati wa miradi ya maji vijijini, kusoma Dira za maji na kufanya Usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji vya Kipule, Mkonganage, Likombora na Ndunyungu.

1.0 UTEKELEZAJI WA HUDUMA YA MAJI VIJIJINI.

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba 2016, shughuli mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maji na ukarabati wa visima vya maji zilifanyika;-

1.1 UKARABATI WA MIRADI YA MAJI VIJIJINI

1. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Kiangara ambapo kilichofanyika ni kufunga "***Push rod"*** mpya na kuondoa iliyokatika katika kisima cha Nalundumbi.
2. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Litou ambapo kilichofanyika ni kufunga cheni mpya na kuondoa iliyokatika katika kisima cha Pachani na Mitalula.
3. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Ngongowele ambapo kilichofanyika ni kufunga "***Push rod"*** mpya na kuondoka chakavu.
4. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Kibutuka ambapo kilichofanyika ni kufunga "***Push rod"*** 3 mpya na kuondoka chakavu
5. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Mikunya ambapo kilichofanyika ni kufunga bomba mpya 11 na kuondoka chakavu katika kisima cha Kijiweni (Pacha ya Sekondari).
6. Ukarabati wa Mradi wa Maji wa mtandao wa bomba kijiji cha Mpigamiti ambapo kilichofanyika ni kubadilisha ***"oil"*** na ***"Filter".***
7. Ukarabati wa Mradi wa Maji wa mtandao wa bomba kijiji cha Namihu ambapo kilichofanyika ni kubadilisha ***"oil"*** na ***"Filter".***
8. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Mirui ambapo kilichofanyika ni kufunga ***"Push rod"*** mpya na kuondoa iliyojifungua kwenye Pampu.
9. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Lineng'ene ambapo kilichofanyika ni ubadilishaji wa ***"Housing"*** ya Pampu
10. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Likombora ambapo kilichofanyika ni kufunga Pampu ya umeme yenye uwezo wa kupampu maji lita 3000 kwa saa na kuondoa pampu ya Mkono.
11. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Chimbuko ambapo kilichofanyika ni kuondoka bomba 3 zilizotoboka katika kisima cha Nambunju.
12. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Liwale B ambapo kilichofanyika ni kufunga "push Rod" mbili mpya na kuondoa zilizokatika.
13. Ukarabati wa kisima katika Kijiji cha Kuchochorokana ambapo kilichofanyika ni kubadilisha ***"Push rod"*** iliyokatika na kufunga mpya.

1.2 MIRADI YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (NRWSSP).

Taarifa ilieleza kuwa utekelezaji wa Miradi ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini inayofadhiliwa na Benki ya Dunia na wahisani ipo katika hatua mbali mbali.

(i) Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya maji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia

- Ujenzi wa miundombinu ya maji katika kijiji cha Likombora.
  Mradi huu upo katika hatua ya usanifu
- Ujenzi wa miundombinu ya maji katika kijiji cha Ndunyungu.
  Mradi huu upo katika hatua ya usanifu
- Ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji vya Kipule na Mkonganage.
  Mradi upo katika hatua ya usanifu.

(ii) Miradi inayotekelezwa na wahisani mbalimbali

- Katika kipindi cha robo ya pili Uchimbaji na ufungaji wa pampu za Mkono katika vijiji vya Mirui, Lineng'ene, Makata na Kipule Magereza umefanyika na kukamilika kwa asilimia 100 na wananchi wameanza kutumia**.** Mradi huu umefadhiliwa na kampuni ya GODRILLING INTERNATIONAL COMPANY LIMITED

2.0 UTEKELEZAJI WA UTOAJI WA HUDUMA YA MAJI MJINI LIWALE

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha Mwezi Oktoba hadi Disemba 2016 Shughuli zifuatazo zilitekelezwa;-

- Ukataji wa huduma ya maji kwa wateja ambao wanamalimbikizo ya madeni ya Ankra za maji umefanyika.
- Usomaji wa dira za maji na uaandaji wa Ankra za maji umefanyika
- Uzibaji wa mivujo ya maji (leakage) kwenye bomba zinazopeleka maji kwa wateja.
- Usafishaji wa Mto Liwale ili kuongeza kasi ya mtiririko wa maji katika chanzo umefanyika

3.0 CHANGAMOTO

Taarifa ilieleza kuwa katika robo ya Pili Oktoba hadi Disemba 2016 Idara imekutana na changamoto zifuatazo:-

- Wananchi kuharibu miundombinu ya maji na vyanzo vya maji hasa Mto liwale
- Wananchi hawachangii huduma ya maji vizuri vijijini/ kutochangia kabisa, inayopelekea baadhi ya miradi ya maji kukosa fedha za kufanyia matengenezo
- Jumuiya kutosimamia vizuri Miradi na kushindwa kuleta taarifa za kila wiki za Mapato na Matumizi.

4.0 MIKAKATI

1. Kutoa elimu ya uchangiaji wa miradi kila wakati
2. Kuandika maandiko ya miradi ya maji
3. Kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji na kuwaondoa wote wanaofanya shughuli zozote zinazopelekea uharibifu wa mto ndani ya Mita 60
4. Kutoa elimu juu ya usimamizi wa miradi ya maji na kuhakikisha huduma hii inawafikia wananchi kwa wakati.
5. Kuhakikisha taarifa za Mapato na Matumizi ya kila wiki, Mwezi na Robo yanapatikana.
6. Kuhakikisha kamati ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Wilaya inafanya shughuli zake ikiwemo kusimamia utunzaji wa vyanzo vya maji.

Taarifa ilipokelewa.

Mjumbe mmoja alieleza kuwa hali ya upatikanaji wa maji kiwilaya ni mbaya na Kata ya Ngongowele ni mbaya zaidi, kuna mabomba tisa hayatoi maji hivyo mjumbe huyo alitaka kujua ni lini Kata ya Ngongowele itapata huduma ya maji.

Maelezo yalitolewa kuwa kisima kimoja kinaleta shida lakini jitihada zinaendelea ili kuhakikisha kisima hicho kinatoa huduma ya maji. Aidha Bwana Scott ameahidi kusaidia kuchimba visima vipatavyo mia moja na kipaumbele cha kwanza kitakuwa Kata ya Ngongowele, Hospitali ya Wilaya na shule zote za sekondari wilayani zitapata huduma hiyo.

6. IDARA YA USAFISHAJI NA MAZINGIRA.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazingira aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Idara ya Usafishaji na Mazingira. Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba , 2017 Idara iliendelea na kazi za usafishaji wa mji kwa kufanya kazi za usafishaji wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali kwa kukusanya na kuzoa taka kwenye maeneo mbalimbali kwa kufuata ratiba iliyojiwekea. Pia Idara imeendelea kutekeleza maagizo mbalimbali yaliyotolewa na viongozi ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya. Maeneo yafuatayo yamefanyiwa kazi kipindi hiki;-

- Soko kuu
- Barabara kuu kutoka Bomani kuelekea Polisi
- Stendi kuu ya magari ya abiria na
- Maeneo kuzunguka uwanja wa mpira
- Hospitali ya Wilaya.

UZOAJI TAKATAKA

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi hiki cha Oktoba hadi Disemba 2016, Idara imeendelea kufanya kazi ya kuzoa taka katika vizimba vya soko kuu, Nangando na Likongowele.. Katika kipindi hiki jumla ya tani 112 za taka ngumu zilikusanywa na kupelekwa dampo.

UTEKELEZAJI WA AGIZO LA MHE. RAIS LA KUFANYA USAFI WA MAZINGIRA JUMAMOSI YA MWISHO WA KILA MWEZI.

Halmashauri ya Liwale imeendelea kutekeleza kikamilifu agizo la Mh. Rais la kufanya usafi wa mazingira siku ya jumamosi ya mwisho ya mwezi, Katika kipindi hiki maeneo yote yaliyoainishwa (Uwanja wa mpira, Soko kuu, Stendi kuu, barabara ya kutoka bomani hadi boma la zamani, Boma, hospitali ya wilaya,Taasisi mbalimbali na Makazi ya wananchi) yamekuwa yakifanyiwa kazi. Zoezi hili ni endelevu na litakuwa linaendelea kila siku ya jumamosi ya mwisho wa mwezi kama serikali ilivyoagiza.

UKAGUZI WA MAJENGO YA BIASHARA.

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi hiki cha Oktoba hadi Disemba 2016 Ukaguzi wa majengo mbalimbali ya biashara ulifanyika ili kubaini mapungufu ya kiafya yaliyojitokeza kwa kuendesha biashara hizo na Idara ilitoa maelekezo kwa Wahusika wa Biashara hizo kwa lengo la kuboresha huduma na kulinda afya za wananchi. Baadhi ya wafanyabiashara ambao walionekana wana matatizo kwenye biashara zao wamepewa muda wa marekebisho kama jedwali lifuatalo linajieleza :-

Jedwali Na:1

NA	AINA YA JENGO/SHUGHULI/SHULE/NYUMBA YA BIASHARA	IDADI YA MAJENGO YALIYOKAGULIWA	MAJENGO YASIYOKUWA NA MATATIZO	MAJENGO YENYE MATATIZO	MAJENGO YALIYOPEWA ONYO/ILANI YA MAREKEBISHO	MAJENGO YALIYOFUNGWA
1	Masoko	1	0	0	0	0
2	Bar/Grocery	3	0	3	3	0
3	Nyumba za kulala wageni	8	0	8	8	0
4	Baba/Mama Lishe	34	0	34	34	0

Majengo yaliyogundulika kuwa na matatizo wakati wa ukaguzi yamepewa muda wa kati ya siku kumi na nne (14) kutoka tarehe aliyokaguliwa ili kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza.

UKAGUZI WA VYAKULA

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba 2016 ukaguzi wa vyakula ulifanyika katika maeneo mbalimbali ili kubaini kasoro za kiafya na kutoa elimu ya kurekebisha kasoro hizo kwa wauzaji na wamiliki wa biashara hizo. Kwa ufafanuzi jedwali lifuatalo linajieleza:-

Jedwali Na:2

NA.	MUHUSIKA/MUUZAJI	ENEO LA BIASHARA	BIDHAA ISIYOFAA ILIYOKAMATWA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
1	Swalehe Saidi Somboko Leseni Na.B 112779205	Likongowele	Soda 26 ml 1000 za take away kampuni ya cocacola na siagi kopo 4, biscuit, azam juisi 59ml 300 na Juisi ya minute mind chupa 12	Ushauri umetolewa juu ya miundombinu ya utunzaji wa bidhaa na bidhaa zilizokamatwa zimeteketezwa kulingana na taratibu za kisheria.sheria ya udhibiti wa chakula,dawa na vipodozi ya mwaka 2003 kifungu Na.34 (1).
4	Hamidu Wamu Leseni Na. B 01413515	Likongowele	Hakuna	Ushauri umetolewa juu ya miundombinu ya duka pamoja na jengo la stoo na utunzaji wa vyakula.
6	Maslahi Saidi Lyuu, B.1954116	Likongowele	Hakuna	Ushauri umetolewa juu ya miundombinu ya duka pamoja na jengo la stoo na utunzaji wa vyakula.

Wafanyabiashara wameelimishwa juu ya upangaji wa bidhaa kwenye stoo zao, bidhaa ya kwanza kuingia stoo ndiyo iwe ya kwanza kuuzwa.

MAFANIKIO

Katika kipindi hiki mafanikio yafuatayo yamepatikana

1. Wafanyabiashara wanaendelea kutekeleza maagizo mbalimbali ya usafi wa mazingira kwenye biashara zao
2. Katika maeneo ya stendi na soko kuu yameendelea kuwa safi kutokana na kudhibiti taka zinazozalishwa katika maeneo haya.
3. Wananchi wanashiriki kikamilifu kwenye shughuli za usafi kila jumamosi za mwisho wa mwezi.

CHANGAMOTO ZILIZOPO.

Katika kipindi hiki changamoto zifuatazo zimejitokeza

1. Upungufu mkubwa wa watumishi wa kada ya afya mazingira
2. Uelewa mdogo kwa baadhi ya wananchi juu ya elimu ya usafi wa mazingira.

MIPANGO YA BAADAYE

Katika kuondoa au kupunguza changamoto zilizoko, Idara imeandaa mikakati ya kupunguza changamoto zilizopo ,

1. Kuendelea kutoa elimu juu ya usafi wa mazingira na kufanya ukaguzi wa usafi wa mazingira kwenye jamii.
2. Kuendelea kufanya ukaguzi wa usafi wa mazingira mara kwa mara kwenye biashara , taasisi na makazi ya watu.

Taarifa ilipokelewa.

KWENDA: BARAZA LA HALMASHAURI
KUTOKA: KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI WILAYA
TAREHE: 31/01/2017 - 01/02/2017

TAARIFA YA KAMATI YA UKIMWI (CMAC) KWENYE BARAZA LA HALMASHAURI TAREHE 31 - 01/02/2017

Mheshimiwa Mwenyekiti,
Kamati ya Kudhibiti UKIMWI katika kikao chake cha kawaida kilichofanyika tarehe 13/10/2017 ilipokea na kujadili taarifa zifuatazo:-

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KUPAMBANA NA KUZUIA MAAMBUKIZI YA VVU/UKIMWI SEHEMU YA KINGA NA TIBA KWA KIPINDI CHA KUANZIA OKTOBA HADI DISEMBA 2016.

Taarifa ilieleza kuwa ili kufikia shabaha ya kuwa na Tanzania yenye Maambukizo mapya 0, Unyanyapaa na Ubaguzi 0, Vifo vitokanavyo na UKIMWI 0, Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii hufanya shughuli za kutoa elimu ya mapambano ya kuzuia na kudhibiti maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI na Idara ya Afya hufanya shughuli za kitabibu. .

Mapambano ya kuzuia na kudhibiti maambukizi ya VVU/UKIMWI yamegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni kinga ambayo hulenga mwitikio wa kijamii na sehemu ya pili hulenga mwitikio wa kitabibu. Mwitikio wa kijamii hushughulikia masuala ya elimu na hamasa kwa jamii kujitokeza kupima afya, kujilinda na maambukizi, kuwajali watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, kuzingatia njia za kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI.Sehemu ya pili ambayo ni tiba hulenga mwitikio wa kitabibu ambao kushughulikia matibabu ya watu wanaoishi na Virisi vya UKIMWI na magonjwa nyemelezi.

2. 0 SHUGHULI ZILIZOFANYIKA SEHEMU YA KINGA
Kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba 2016, Idara ya Maendeleo ya Jamii imetekeleza shughuli zifuatazo;

2.1 KUJENGA UWEZO WA KLABU ZA UKIMWI ZA SEKONDARI 16 KUTEKELEZA MALENGO YA KLABU

Kusimamia na kuwezesha klabu za UKIMWI za shule za sekondari kuanzisha shughuli na miradi yenye kuwawezesha kutumia muda vizuri na vile vile kupata elimu ya kukabiliana na maambukizi ya VVU/UKIMWI ili Tanzania iweze kuwa na kizazi kipya chenye uwezo wa kufikia malengo ya kuwa na **maambukizi 0**, **vifo vitokanavyo na UKIMWI 0** na **Unyanyapaa 0**, na hatimaye wanafunzi waweze kuwa mabalozi wa mabadiliko katika familia zao, na kwa vijana wenzao walio nje ya shule.

Kundi la Wanaafunzi lina wanawajibu wa kuhakikisha kuwa kizazi kipya hakitakuwa na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI kwa kuwezeshwa '**Vijana kupata maarifa na ujuzi wa kutosha wa kujikinga wao wenyewe na wenzao dhidi ya kuenea kwa UKIMWI**." *Sera ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI 2001*"

Klabu ya shule ya Nicodemus Banduka ilijengewa uwezo wa kitaaluma wa kuandaa miradi yenye kuhamasisha vijana kuendelea kuwa pamoja baada ya muda wa masomo, kujadili changamoto za ujana na njia za kushinda changamoto za mabadiliko ya mwili ambazo hupelekea vitendo vya ngono.

Aidha Klabu ya Nicodemus Banduka baada ya kujengewa uwezo, imemudu kuanzisha miradi 2 ambayo ni mradi wa Ufugaji wa Kuku na bustani ya Upandaji miti. Mpango huu wa kuanzisha miradi utaendelea katika shule ya Sekondari ya Kibutuka na hatimaye shule nyingine za sekondari zitafuatia mara baada ya kufunguliwa kwa shule za sekondari

Aidha wakati wa kusimamia na kujenga uwezo wa Klabu za Kupinga na Kuzuia Maambukizi Mapya ya VVU/UKIMWI, wanafunzi wa walielimishwa na masula ya kijinsia na VVU/UKIMWI ambayo ni :-

i. Kukabiliana na tabia ya kundi rika la vijana- Wanafunzi walishirikishwa na kujadili namna ya kukabiliana na changamoto za ujana kwa kutumia mbinu zifuatazo :-

a) Vijana kuepuka kujiunga katika makundi hatarishi yakiwemo ya wacheza kamari, wezi na wavuta bangi.

b) Vijana kujenga tabia ya kujiunga na vikundi vya kufanya mazoezi ya viungo ikiwemo kucheza mpira, riadha,kucheza ngoma, na mazoezi ya viungo.

2.2 KUTOA ELIMU YA MAPAMBANO YA KUZUIA MAAMBUKIZI YA VVU/UKIMWI KWA VIKUNDI VYA KILIMO CHA UMWAGILIAJI KATA YA MANGIRIKITI NA UFUGAJI WA SAMAKI BARIKIWA

Taarifa ilieleza kuwa vikundi vinawajibu mkubwa wa kuelimisha jamii kupitia umoja hasa kwa kusimamia masula mbalimbali yanayowazunguka ikiwemo na masuala ya mapambano ya Kuzuia na Kudhibiti Maambukizi Mapya ya VVU/UKIMWI kwa wao wenyewe wanakikundi na kwa makundi rika yote na hasa ya vijana na wanawake ambao huhitaji kulindwa na kuwawezesha kutambua athari za maambukizi ya VVU/UKIMWI na jinsi ya kutambua na kukabiliana na ukatili wa jinsia.

Vikundi vya Kilimo cha Umwagiliaji Mangirikiti na Ufugaji wa Samaki vilielimishwa

a) Kuacha kabisa tabia kuwa na wapenzi wengi

b) Kila mzazi atenge muda wa kufuatilia tabia za vijana ili kuwalinda watoto wakike na vijana kutojiingiza katika matendo ya kujamiia

c) Kushirikiana na serikali za vijiji vyao kuwaepusha vijana na mazingira hatarishi ikiwemo maeneo ya vileo na madawa ya kulevya na kucheza mchezo wa "pool table".

2.3 KUTOA ELIMU YA MAPAMBANO YA KUZUIA NA KUDHIBITI MAAMBUKIZI MAPYA YA VVU/UKIMWI KATIKA MAENEO YALIYO PITIWA NA MIRADI YA UJENZI WA BARABARA ZA MAKATA –NDAPATA NA LIWALE KIKULYUNGU

Taarifa ilieleza kuwa Idara ya Ujenzi kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii, iliwezesha utoaji elimu ya mapambano ya kuzuia na kudhibiti maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI katika maeneo yaliyo pitiwa na mradi wa ujenzi wa barabara za Liwale –Kikulyungu na Makata- Ndapata kwa njia Sinema.Vijiji vilivyo pata elimu hii ni Kikulyungu na Mlembwe. Aidha Elimu iliyotolewa kwa njia ya SINEMA ilikuwa ni pamoja na:-

i. Madhara ya kuwa na wapenzi wengi.
ii. Kuhimiza jamii kutofanya matumizi ya pamoja ya vitu vyenye incha kali ikiwemo nyembe, sindano na mikasi.
iii. Kuhimiza jamii kuwa na tabia nzuri za kujamiiana kwa usalama zaidi, kuwa na wenza waaminifu, kufanaya mapenzi kwa kutumia kondom
iv. Kuwahi kutibu magonjwa yazinaa katika vituo vya afya na kufanya uchunguzi mapema wa maambukizo ya UKIMWI kwa kupatiwa ushauri na nahasa.
v. Wazazi na Walezi kufuatilia tabia na malezi ya vijana wao walio mashuleni na wasio mashuleni ili wasijiingize katika katika matendo ya ngono ambayo husababisha maambukizo ya VVU/UKIMWI, magonjwa ya zinaa na mimba za utotoni na zisizo tarajiwa .

Vile vile wakati wa jioni , kabla ya kuanza kuoneshwa SINEMA wananchi waliweza kusikiliza matangazo yenye ujumbe wa

a. Kupinga na kuzuia unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.
b. Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI wanastahili kupata mahitaji yote ya msingi na haki zote za raia, za sheria na binadamu bila ya Ubaguzi wowote wa kijinsia au hali
c. Watu wanaofuata ushauri nasaha, matibabu na matunzo ya VVU/UKIMWI wataendelea kupatiwa haki sawa na mtu mwingine yeyote anayehitaji huduma nyingine za afya na vile vile taarifa za mtu anaishi na VVU/UKIMWI zitaendelea kuwa za siri hadi pale atakapojitangaza.

3.0 SHUGHULI ZA MAPAMBANO DHIDI YA VIRUSI VYA UKIMWI SEHEMU YA TIBA

Taarifa ilieleza kuwa Idara ya Afya bado inaendelea na mapambano ya siku hadi siku ya kupunguza kasi ya maambukizi mapya kutoka 2.0% iliyopo kwa sasa hadi kufikia 0%. Kwa kuzingatia hilo tiba na elimu mbalimbali zinatolewa na watoa huduma kwa wateja tunaowahudumia. Elimu inayotolewa ni pamoja na kujikinga kwa wale walioambukizwa wasiambukize wenzao na wale ambao hawajambukizwa waendelee kujikinga ili wasiambukizwe. Elimu hii inatolewa kila sehemu ya hospitali pale tu mteja atakapohudumiwa shida iliyomfanya afike hospitali baadae anapatiwa elimu ya ziada ya jinsi ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI (ushauri nahasa) na ikiwezekana kupimwa kabisa Afya kwa wale ambao hawazitambui hali zao kiafya.

Ushauri Nasaha na kupima virusi vya UKIMWI

Huduma hii ilianza mwaka 1996 katika kituo kimoja ambacho ni Hospitali ya wilaya. Sasa hivi inatolewa katika vituo 33. Pia vituo vyote 33 vinatoa huduma Shawishi na Upimaji pamoja na huduma ya kuzuia maambukizi ya virusi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Kuanzia Mwezi Oktoba hadi Disemba 2016, jumla wateja walijitokeza kupima kwa hiari 2011, kati yao 37 sawa na asilimia 1.8 waligundulika kuwa na maambukizi, na wote waliandikishwa katika vituo vya tiba.

Jedwali kuonesha upimaji na usajili wa wateja kipindi cha Oct-Dec 2016

Wateja	Me	Ke	Jumla
Idadi ya waliopimwa	499	1512	2011
Idadiya Waliombukizwa	9	28	37
Idadiya waliosajiliwa	9	28	37

Kuzuia Maambukizi toka kwa Mama Kwenda kwa Mtoto (PMTCT)

Mpango wa kuzuia maambukizi toka kwa mama kwenda kwa mtoto ulianza rasmi Mwaka 2006, na kulikuwa na kituo kimoja tu cha kutolea huduma hii ambacho Hospitali ya wilaya ya Liwale. Mpaka sasa ni Vituo vyote 33 vinavyotoa huduma hiyo. Kiwango cha maambukizi kwa akina mama wajawazito waliojitokeza kupima Mwaka 2012 kilikuwa ni 1.7%. Kiwango hiki kimeendelea kupungua mpaka kufikia asilimia 1.4 Desemba 2016. Katika kipindi cha Oktoba-Disemba 2016 idadi ya wajawazito waliopima VVU ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini

Kiwango cha maambukizi kwa akina mama wajawazito

Mwaka	Idadi ya wajawazito waliopimwa VVU	Idadi ya wajawazito wenye maambukizi	Kiwango cha maambukizi katika (%)
Okt- Disemba 2016	261	8	1.4

Wateja wanaotumia Dawa.

Taarifa ilieleza kuwa kuanzia tarehe 1 Oktoba 2016 Wizara ya Afya kupitia NACP (MPANGO WA TAIFA WA KUDHIBITI UKIMWI) ilitoa muongozo mpya wa matibabu na malezi kwa wagonjwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI kuwa kila mteja

anayepatikana na maambukizi ya VVU ataanzishiwa dawa za kufubaza makali ya VVU(ARVs) mara moja bila kuzingatia wingi au uchache wa kinga za mwili(CD4) count, hivyo basi kuanzia tarehe hiyo mpaka sasa tunaendelea kutoa huduma kufuata muongozo huo. Vile vile tumeendelea kuwaanzishia dawa wateja wote ambao wapo katika huduma lakini bado walikuwa hawajaanza dawa kutokana na muongozo wa awali uliotutaka kuanzishia dawa wale tu ambao waliokuwa na kinga mwili chini ya 500.g/dl. Hivyo basi jedwali hili hapa chini linaonesha wale wateja wapya na wale wa zamani walioanzishiwa dawa katika kipindi hiki cha Okt- Dis 2016

Jumla ya wateja wapya 37 kati yao wanaume ni 9 na wanawake 28 tulifanikiwa kuwaingiza katika huduma pamoja na kuwaanzishia dawa moja kwa moja kama mwongozo unavyoeleza, pia jumla ya wateja 64 kati yao wanaume 11 wanawake 52 ambao walikuwa kwenye huduma hapo awali tuliweza kuwashawishi na kuwapa elimu juu ya mwongozo mpya ambao unawataka kuanza dawa hivyo kwa kipindi cha Oktoba-Disemba 2016 Jumla ya wateja 101 walianzishiwa dawa za kufubaza makali ya VVU.

Mwaka	Idadi ya wanaume waliopo kwenye	Idadi ya wanawake waliopo kwenye dawa	Jumla kuu
Okt- Disemba 2016	585	1470	2055

Bado tukabiliwa na tatizo la wateja wengi kukataa kuanzaa kutumia dawa kama mwongozo mpya unavyotaka lakini bado tunajitahidi kutoa elimu kila siku juu ya umuhimu
wa kuanza dawa mapema na faida zake.

HUDUMA MBALIMBALI ZINAZOENDELEA KUTOLEWA KWA WATEJA WANAOISHI NA VVU

Ili kuhakikisha Afya za wateja wetu zinaimarika bado tunaendelea kupima wingi wa kinga za mwili (CD4) Count japokuwa katika swala la kuanzisha dawa hatuzingatii wingi au uchache wa kinga za mwili, tunafanya hivi ili kuangalia ufanisi wa dawa wanazotumia wateja wetu ikitarajiwa kuwa ndani ya miezi sita(6) tunategemea kinga za mwili ziongezeke kama masharti na maelekezo aliyopatiwa mteja wetu atayafuata kama alivyoelekezwa, pia pale ambapo tutaona matokeo ni kinyume na matarajio yetu basi tatuwezesha kujua kuwa dawa alizopewa mteja hazimsaidii hivyo tutaweza kumbadilishia na kumpa dawa nyingine.

IDADI YA WATEJA WALIOPOTEZA MAISHA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA-DISEMBA 2016

Wanaume	Wanawake	Jumla
2	1	3

IDADI YA WATEJA WALIOACHA HUDUMA NA KUFANIKIWA KUWARUDISHA TENA KATIKA HUDUMA

Wanaume	Wanawake	Jumla
1	3	4

Taarifa ilieleza kuwa idadi ndogo ya wateja tulifanikiwa kuwarudisha katika huduma imetokana na kukosekana kwa wasaidizi wetu waliokuwa wanatusaudia katika zoezi la ufuatiliaji kwa wateja waliocha kuhudhuria katika kliniki zetu. Wasaidizi hawa wlikosekana tangu mwezi wa tisa pale tu EGPAF walipositisha kufadhili shughuli za UKIMWI wilayani Liwale hivyo na wao mikataba yao ndipo ilipoishia.

CHANGAMOTO

1. Utoro wa wateja katika huduma hii inachangiwa na shughuli mbalimbali za Kilimo
2. Vifo visivyoripotiwa husababisha mteja kuonekana mtoro kumbe alishafariki
3. Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza baadhi ya shughuli za mapambano dhidi ya VVU.

Taarifa ilipokelewa.

Wajumbe walitoa hoja kuwa zitafutwe changamoto za kubaini kwa nini wateja wanatoroka, pia wajumbe hao walisisitiza kuwa waonekane ndani ya taarifa na waonane na wanakamati husika.

Hoja hiyo ilielezwa kuwa kinachotakiwa ni mteja anayepata huduma ile kuaga katika kituo husika (kutoa taarifa) pia wafadhili watakuja kuonana na Kamati.

Mustafa Y. Mtegite
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI